



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA  
BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA**



**TANGAZO KWA UMMA**

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) ni taasisi chini ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara iliyoundwa kwa Sheria Namba 10 ya Mwaka 2005 na Marekebisho Kifungu cha 4 Sura ya 339 R.E. 2016. Bodi imepewa majukumu chini ya Kifungu 5 (a-j) ya Sheria hiyo ikiwemo kutoa leseni kwa Waendesha Ghala, Meneja Dhamana na Wakaguzi wa Ghala.

Katika kuelekea msimu wa mauzo ya Ufuta 2021/2022; Bodi inapenda kuutarifu umma kuwa itapokea maombi ya leseni za Waendesha Ghala kwa zao la Ufuta kwa Mikoa yote nchini inayozalisha Ufuta.

Pamoja na mambo mengine yaliyoainishwa Sehemu ya IV ya Sheria ya Stakabadhi za Ghala kuhusu utaratibu wa utoaji leseni, waombaji wanatakiwa kuzingatia yafuatayo: -

- i. Kuwa na kipima unyevu ambacho kimefanyiwa ugenzi (calibration) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS);
- ii. Mzani wa kupimia Ufuta uliyothibitishwa na Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA);
- iii. Mizani midogo ya kupimia sampuli iliyothibitishwa na Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA);
- iv. Kuweka Kinga ya Utendaji ya aidha 'Bankers Guarantee' au 'Insurer's guarantee';
- v. Kujaza Fomu Namba 1 na 2 kikamilifu na kuweka viambatisho husika;
- vi. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 20 Aprili 2022;
- vii. Ada ya maombi ni Shilingi 20,000 kwa ghala;
- viii. Maombi yatakayochelewa mwombaji atatozwa adhabu ya kugharamia ukaguzi wa ghala zake (malipo yote yatafanyika kupitia Mfumo wa Kieletroniki wa Malipo ya Serikali);

Imetolewa,

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji

01 Aprili 2022